# KUHAMISHWA KWA HISA ZILIZOORODHESHWA KATIKA SOKO LA HISA LA NAIROBI (NSE)

CDSC
CENTRAL DEPOSITORY & SETTLEMENT CORPORATION LIMITED

# Tukio la kihistoria biashara ya hisa ikiacha kutumia karatasi

**Na EVANS ONGWAE**
eongwae@ke.nationmedia.com

Novemba 2013, sawa na Novemba tisa zilizopita, ni wakati wa kuandikisha historia katika masoko ya mtaji Kenya. Ndio mwezi ambao vyeti vya hisa vya karatasi vitaacha kutumika, na kupeleka masoko ya mtaji katika ngazi nyingine.

Central Depository & Settlement Corporation Limited (CDSC), kufuatia mashauriano na kampuni zilizoorodheshwa kwenye soko la hisa, Mamlaka ya Masoko ya Mtaji na Soko la Hisa la Nairobi (NSE) iliweka Novemba 2013 kuwa siku ya mwisho ya kuhamishwa kwa hisa zote zilizoorodheshwa kwenye soko la hisa.

Shughuli hii, kwa Kiingereza, dematerialization, huhusisha kubadilishwa kwa vyeti vyote vya hisa vilivyo kwenye karatasi na kuwa za elektroniki, tofauti kuu ikiwa kwamba siku iliyotengwa ya kuhamishwa, hisa zote zitakuwa kwenye mfumo wa kielektroniki na vyeti vya karatasi vitakoma kutumika kama ushahidi wa umiliki wa hisa katika kampuni yoyote ile ambayo hisa zake zimeorodheshwa katika Soko la Hisa la Nairobi (NSE). Ushahidi wa umiliki utakuwa orodha ya kielektroniki ambayo itakuwa kwenye Central Depository System (CDS) kisimamiwa na CDSC.

Kuambatana na Kifungu 7 cha Sheria ya Central Depositories ya 2000, wote wanatoa hisa zilizoorodheshwa kwenye soko la hisa wanafaa kutoa ilani au notisi kwa wenyehisa wao mara moja kwa wiki kwa kipindi cha wiki tatu mfululizo kabla ya tarehe ya kuhamishwa kwa hisa.

Afisa Mkuu Mtendaji wa CDSC Rose Mambo hata hivyo, alifafanua kuwa wenyehisa ambao tayari wameweka hisa zao zote kwenye CDS hawatahitajika kuchukua hatua nyingine yoyote kufuatia hatua hii ya kuhamisha hisa. "Ikiwa bado unaendelea kushikilia vyeti vyako vya hisa, unashauriwa utembelee, benki yako ya uwekezaji, wakala wa hisa au anayekuhifadhia hisa na ufungue akaunti ya CDS ambapo utaweza kuweka hisa zako. Hisa zote ambazo hazitakuwa zimehamishwa kufikia tarehe hiyo ya kuhamisha hisa zitaonyeshwa katika depo ya hisa zikiwa na jina la mwenyehisa akisubiriwa afungue akaunti ya CDS," alifafanua.

Hatua ya kuhamisha hisa inafuatia shughuli ya miaka tisa iliyofanikiwa ya kusitisha matumizi ya vyeti vya hisa vya karatasi iliyoanza 2004.

Mwaka 2012, katika hatua ya kufuatiliza ufanisi wa shughuli hii, CDSC ilianza shughuli ya kuhamisha his azote ambazo zimeorodheshwa kwenye soko la hisa, na imeandaa warsha kadha na wadau kuhusiana na hili. Kadhalika, kuanzia siku hiyo kwenda mbele, vyeti vya hisa vya karatasi vitakoma kutambuliwa kama ushahidi wa umiliki wa hisa, na rekodi za kielektroniki katika CDS zitakuwa ndizo mwamuzi wa umiliki wa hisa. Aidha, kuanzia siku hiyo, hakuna kampuni yoyote iliyoorodheshwa ambao itawapa wenyehisa wake vyeti vya umiliki wa hisa na badala yake maelezo yatawekwa kielektroniki katika CDS yakiwa na jina la mwenyehisa. Kuna jumla ya kampuni 63 zilizoorodheshwa katika NSE.

Shughuli ya kusitisha matumizi ya vyeti vya karatasi ilianza 2004 pale Central Depositories & Settlement Corporation Limited ilipoundwa.

Shirika hilo lilianzisha Central Depository System, ambao ni mfumo wa kompyuta ambao hufanikisha kuhifadhiwa kwa hisa katika akaunti za kielektroniki na kufanikisha uuzaji na ununuzi haraka na rahisi katika NSE. CDS inawahakikishia wadau ununuzi na uuzaji wa kasi, salama na rahisi wa hisa.

Shughuli ya kusitisha matumizi ya vyeti vya karatasi ilianza kwa awamu mwaka 2004, ambapo kampuni zilizoorodheshwa ziligawanywa mara nne, na CDSC ikawa ikitangaza kwa kusonga wakati wa utekelezaji wa shughuli hiyo katika kila kikundi, maana kuwa kuanzia siku hiyo, vyeti hivyo vingewasilishwa na pahala pake kuchukuliwa na rekodi ya kielektroniki ya umiliki huo ambao unaitwa kiingilio katika kitabu. Hii ilikuwa pia na maana kuwa hakuna hisa au hati ya thamana ambayo ingeuzwa bila kuwa katika hali hiyo.

Kufikia Februari 2005, hisa zote zilizoorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Nairobi zilikuwa zimehitimu kuhamishwa, na uuzaji na ununuzi katika soko ambao ulifanywa kuanzia wakati huo ulifanywa kwa kutumia hisa za viingilio kwenye vitabu. Jumla ya asilimia 83.85 ya hisa zote huru zilikuwa zimepitia shughuli hii na asilimia 54.58 ya jumla ya his azote zokoni zilikuwa zimefanyiwa hivi kufikia 23 Mei 2013 ikiwa ni za thamani ya Sh.954.7 bilioni kufikia tarehe hiyo. Hati za thamana zilizowekwa kwenye mfumo wa kielektroniki kufikia 23 Mei 2013 zilikuwa asilimia 63.90 ya thamani ya hati zote sokoni.

Mfumo wa CDS, ambao ulinunuliwa kutoka kwa Millennium Information Technologies Limited of Colombo, Sri Lanka, ulizinduliwa kwa matumizi 10 Novemba 2004.

Utekelezaji wa Central Depository System ni mradi halisi wa kitaifa na manufaa yanayotokana na ufanisi wake yatawafaa wawekezaji wote Kenya. Ulibadilisha sana jinsi shughuli hufanywa katika soko la hisa na hivyo ni muhimu sana kwa umma kufahamu unavyofanya kazi.

Haya yote yalianza baada ya Bunge kupitisha Sheria ya Central Depositories ya 2000. Mengine, kama inavyosemwa, ni historia.

Kipindi hicho cha miaka tisa ya kusitisha matumizi ya vyeti vya hisa vya karatasi shughuli ambayo kilele chake ni kuhamishwa kwa hisa, CDSC imechukua hatua kuu kuhakikisha usalama wa hisa za wenyehisa. Kampuni hiyo ina mifumo ya ziada ya kuweka maelezo yote na taratibu kuhakikisha kuendelea kwa biashara kukitokea jambo lolote la kuathiri mfumo wa kompyuta unaotumiwa au kuathiri afisi zake. CDSC imechukua tahadhari kuhakikisha mfumo huo hauingiliwi na kuhujumiwa.

Pamoja na haya, CDSC imeajiri wafanyakazi wenye viwango vya juu vya maadili na ambao hudumiwa viwango vya juu sana vya usiri.

"Utekelezaji wa Central Depository System ni mradi halisi wa kitaifa na manufaa yanayotokana na ufanisi wake yatafaa wawekezaji wote Kenya.

> **"Utekelezaji wa Central Depository System ni mradi halisi wa kitaifa na manufaa yanayotokana na ufanisi wake yatafaa wawekezaji wote Kenya.**

13 X 6 Collumns Advert

KUHAMISHWA KWA HISA ZILIZOORODHESHWA KATIKA SOKO LA HISA LA NAIROBI (NSE)

# Ufafanuzi wa shughuli za Central Depository and Settlement System

**Na EVANS ONGWAE**
eongwae@ke.nationmedia.com

Central Depository & Settlement Corporation Limited (CDSC) ni kampuni ya dhima yenye ukomo ambayo imeidhinishwa na Mamlaka ya Masoko ya Mtaji chini ya Kifungu 5 cha Sheria ya Central Depositories ya 2000 kuanzisha na kutekeleza mfumo wa kufanikisha uwekaji kwenye depo na ubadilishanaji wa umiliki wa hisa na hati za thamana na malipo ya pesa kufuatia shughuli za kibiashara katika Soko la Hisa la Nairobi.

CDSC ilianzishwa rasmi 23 Machi 1999 chini ya Sheria ya Kampuni na ikaanza shughuli zake kama Mhifadhi Mkuu mnamo 10 Novemba 2004. CDSC ina wenyehisa sita wanaoimiliki: Capital Markets Challenge Fund (asilimia 50), Soko la Hisa la Nairobi (asilimia 22.5), AKS Nominees Ltd. (asilimia 18), Capital Markets Investor Compensation Fund (asilimia 7) na Soko la Hisa la Uganda (asilimia 2.5).

Central Depositories & Settlement Corporation (CDSC) hutekeleza mchango muhimu katika masoko ya mtaji.

Soko la hisa, ambalo hujulikana kama soko la pili na uuzaji na ununuzi ukilinganisha na soko la kwanza ambalo ni mgawo wa hisa kwa umma (IPO), hupokea maagizo kutoka kwa wahusika kama vile mawakala ambao wamepewa idhini mapema na soko ya kushiriki katika mfumo wa kuamua bei. Baadaye hupitisha bei hizo na hisa husika kwa shirika la kukamilisha ununuzi na kufanya malipo ambalo hufanya mipango ya kufanikisha malipo na ubadilishanaji wa umiliki wa hisa. Soko hili huhudumia wanunuzi na wauzaji wa bidhaa hizo na kifedha pamoja na wanaozitoa.

Kote duniani, mifumo ya uhifadhi na ubadilishaji wa umiliki wa hisa husimamia shughuli zote za kibiashara za baadaye ambazo hufanyika katika kaunta zilizopangwa vyema kwenye masoko.

CDS huwajibika katika uidhinishaji wa ubadilishanaji huu wa hisa, hivi kwamba nafasi halisi ya kila mwekezaji inajulikana. CDS zote huwa karibu kila wakati zinawajibika katika ubadilishanaji wa umiliki wa hisa, hivyo ni kusema, malipo na uwasilishaji halisi au kwa njia ya elektroniki wa bidhaa ya kifedha iliyonunuliwa na kuwajibikia shughuli hiyo yote. Kufuatia kuwasilishwa kwa malipo, CDS huhusika katika shughuli ya kusimamia bidhaa hizo za kifedha kwa niaba ya wawekezaji na wanaozitoa. Huduma hizi ni pamoja na usimamizi wa majukumu ya umiliki wa hisa na utambuzi wa wenyehisa wa kampuni.

Shughuli kuu zinazotekelezwa na Central Depository and Settlement System ni:

- Kunakili Shughuli ya Kibiashara/Uhakikishaji
- Uthibitishaji wa Shughuli ya Kibiashara
- Kufanya hesabu (kuamua wajibu wa kila upande katika ubadilishanaji wa umiliki), uwe wa pande mbili au nyingi, ambao unaweza kuhusisha kutolewa kwa cheti kipya (CDS hapo huwa ni kama mthibitishaji wa shughuli hiyo ya kibiashara).
- Malipo
- Mhifadhi Mkuu/Sajili

**ENDELEA UK 8**

# KUHAMISHWA KWA HISA ZILIZOORODHESHWA KATIKA SOKO LA HISA LA NAIROBI (NSE)

## Ufafanuzi wa shughuli za Central Depository and Settlement System

KUTOKA UK 7

Karibu CDS zote kote duniani hulenga kufanikisha mfumo wa Uwasilishaji dhidi ya Malipo (DvP). DvP ni hali kwamba shughuli ya kibiashara ikikamilishwa mwuzaji huwasilisha hisa ibadilishwe umiliki wakati ule ule ambapo pesa zinapokelewa. Huwa kuna shughuli ya mara moja ya pande mbili ya kubadilishana ambayo inakamilika na hakuna uwezekano wa hilo kubadilisha.

DvP inayofanya kazi vyema ni muhimu katika kupunguza hatari ya biashara kwenye kaunta, kwani biashara hukamilishwa upesi bila makosa, kukiwa na uwezekano finyu sana wa malipo kutotolewa.

Kuna aina tatu za hatari ambazo CDS huzuia:

- Hatari ya amana, ambapo hisa au pesa zimewasilishwa lakini upande ule mwingine wa shughuli hiyo ya kibiashara haujakamilishwa.
- Hatari ya gharama ya kurejesha, ambapo shughuli ya kibiashara inakosa kukamilika na lazima shughuli hiyo ibatilishwe.
- Hatari ya ulipaji deni, ambayo ni gharama inayotokana na kucheleweshwa kwa malipo.

Mfumo wa sasa wa uidhinishaji, ubadilishaji wa umiliki na usajili Kenya umekuwa na changamoto nyingi huku soko letu ya mtaji likiendelea kukua. Kuongezeka sana kwa idadi na madeni kunaweza kuongeza hatari katika mfumo wa sasa wa kutumia vyeti vya karatasi hadi viwango ambavyo havikubariki.

Soko la Hisa la Nairobi, kwa ushirikiano na wadau katika soko, lilichunguza mfumo wa sasa kwa makini na kuamua kutekeleza mfumo wa kisasa na thabiti wa uidhinishaji, ubadilishanaji wa umiliki na uwekaji hifadhi wa hisa. Hii itawezesha wawekezaji kuhamisha hisa au hati za dhamana zilizoorodheshwa bila kuhitaji hisa au fomu za kuhamisha au kubadilisha umiliki. Hisa zitawasilisha na akaunti kwenye vitabu ambazo zitahamishwa mara moja kwa kuhamisha kiingilio kwenye kitabu katika akaunti za CDS. Kwa kueleza kwa urahisi, CDS itatoa kwa biashara ya hisa na hati za dhamana yale ambayo benki hutoa kwa biashara ya pesa taslimu – ni hazina salama ya hisa na hati za dhamana.

# CDSC yaimarisha teknolojia yake kuwa ya kisasa ili kufika ngazi nyingine

**Na EVANS ONGWAE**
eongwae@ke.nationmedia.com

Central Depository & Settlement Corporation Limited (CDSC), ambayo imo kwenye njia ya ukuaji inatarajia kutumia teknolojia kuiongoza kufikia ufanisi siku za usoni.

CDSC imo kwenye shughuli na kuimarisha na kufanya wa kisasa, mfumo wake ambao sasa utakuwa ni mtandao thabiti wa muundo mara tatu. Hatua hii inatarajiwa kuimarisha usalama wa mfumo huo, kupitia kutumiwa kwa teknolojia ambao ni rahisi kutumiwa na watu na ambayo itaongeza huduma za kibiashara ambazo CDSC inaweza kutoa katika masoko ya mtaji kuambatana na mpango wake wa mikakati.

Mfumo huo tayari ni thabiti kiasi kwamba unaweza kufanya kazi na kutoa huduma ya uhakika asilimia 99.9 na inatiwa nguvu zaidi na kundi la wataalamu wa IT wenye ujuzi. Mfumo huo ulifanikisha bila matatizo yoyote IPO ya kwanza kubwa zaidi Afrika Mashariki: Mgawo wa Hisa kwa Umma (IPO) wa Safaricom. IPO hiyo ya kampuni kubwa zaidi ya utoaji wa huduma za mawasiliano ya simu ulitoa hisa 10 bilioni za Sh.5 kila hisa – ambayo ni jumla ya hisa za thamani ya Sh. 50 bilioni wakati wa kutolewa kwa IPO hiyo Machi 2008.

CEO wa CDSC anafafanua kuwa kuimarishwa kwa mfumo huo wa IT kunakusudiwa kuimarisha usalama, kupitia kutumiwa kwa teknolojia ambao ni rahisi kutumiwa na watu na ambayo itaongeza huduma za kibiashara ambazo CDSC inaweza kutoa katika masoko ya mtaji kuambatana na mpango wake wa mikakati.

Mhifadhi wa hisa za Kenya CDSC, Bi. Mambo anasema, imefikisha masoko ya mtaji Kenya hadi ngazi nyingine kutokana na utendakazi bora ulitokana na kutumiwa kwa mitambo ya kompyuta jambo ambalo limewezesha mawakala wa hisa na wawekezaji kufanya mengi zaidi – bila kuwepo wenyewe eneo la biashara.

"Ni rahisi sana kuuza au kununua sasa na wawekezaji hawana hofu tena kuhusu vyeti vya hesa," alieleza, na kusema kuwa inasaidia wawekezaji kuleta pamoja hisa wanazomiliki. Aidha, mfumo wa malipo unapunguza utapeli na ulaghai kwani hakuna vyeti ambavyo vinaweza kuibiwa.

Matokeo ya kazi ya CDSC katika masoko ya mtaji Kenya yamechangia sana katika ufanisi ambao umeshuhudiwa katika soko tangu kuanzishwa kwake. Mwaka 2004, ilianza kazi ikiwa na akaunti 30,000 za wateja na jumla ya shughuli 200 za kuuza au kununua katika NSE ambazo zilifanikishwa kupitia Central Depository System (CDS). Leo hii, idadi ya akaunti ya wateja imeongezeka na kufikia 1.97 milioni kufikia Aprili 2013, kukiwa na kiwango cha kadiri cha shughuli za uuzaji au ununuzi cha 2,700 zinazokamilishwa kila siku kupitia mfumo wa CDS.

Fauka ya vyeti vya hisa kufanywa vya kielektroniki, CDSC pia imeshuhudia ufanisi katika maeneo mengine.

### Kuanzishwa kwa Viwango vya Juu vya Malipo

Jukumu kuu la CDSC, linaitaka ifanikishe mikakati thabiti ya kukabili na kuzuia hatari wakati wa malipo kwneye soko. Kuhusiana na hili, viwango vya juu zaidi vya malipo vilianza kutekelezwa kuanzia Januari 2010, kuhakikisha hakuna Ajenti Mkuu Mhifadhi wa Hisa anayeweza kuahidi kwamba atafanya malipo ambayo yako zaidi ya kiwango alichoruhusiwa, bila ya kuwasilisha ushahidi wa atakapotoa pesa za kufanikisha malipo hayo. Hili ni kuambatana na maadili bora ya utendakazi ya wahifadhi wakuu wa hisa katika mifumo ya malipo ya hisa.

### Kuanzishwa kwa Benki Nyingi za Malipo

Mwaka 2012 CDSC iliteua benki tatu zaidi za kufanya malipo. Benki hizo tatu zilizojiunga na CFC Stanbic Bank ni Barclays Bank, Cooperative Bank na Equity Bank. Hili limeimarisha ufanikishaji wa malipo na kusambaza hatari ya kutegemea benki moja kufanikisha malipo. Hili pia huwapa Maajenti Wakuu Wahifadhi wa Hisa benki nyingi za kuchagua wakifanikisha malipo ya mtaji au deni kupitia benki wanayopenda.

# Kufanya hisa kuwa za elektroniki kuinua hadhi ya Kenya

By **EVANS ONGWAE**
eongwae@ke.nationmedia.com

Uamuzi wa kuhamisha hisa zote zilizoorodheshwa katika soko la hisa ni hatua kuu katika soko la mtaji ambayo itainua hadhi ya soko la mtaji la Kenya katika kutii kanuni na maadili ya kimataifa. Haya ni kwa mujibu wa Afisa Mkuu Mtendaji wa Central Depository & Settlement Corporation (CDSC) Rose Mambo. Anaongeza kuwa hatua hii itasaidia sana katika kuimarisha utendakazi na utoaji huduma katika soko la mtaji na soko la hisa.

Soko la Hisa la Nairobi ni soko ambalo huhusika katika uuzaji na ununuzi wa hisa na hati za dhamana zilizotolewa na kampuni zilizoorodheshwa rasmi na pia kutoka kwa serikali.

Mchango mkuu ambao soko la hisa limetekeleza, na linaendelea kutekeleza katika chumi nyingi ni kwamba huendeleza desturi ya kutotumia pesa kiholela, au kuweka akiba. Kwa kuwa taasisi ziko ambapo mwenye kuweka akiba anaweza kuwekeza pesa zake salama na kando na hayo kupata faida, ni kichocheo kwa watu kutumia pesa kidogo na kuweka akiba nyingi.

Soko hili pia husaidia katika kuhamisha akiba hadi kwa uwekezaji katika kampuni zinazoleta faida kama njia mbadala ya kuweka akiba pahala ambapo haileti faida.

Soko la hisa thabiti husaidia katika kusambaza na kutumia vyema mtaji, ambao ni rasilimali adimu. Hali kwamba mtaji ni adimu sana ina maana kuwa mifumo sharti iundwe ya kuhakikisha mtaji unamwendea Yule anayeuhitaji zaidi. Sekta ya soko la hisa inayofanya kazi vyema ina ujuzi huu, taasisi na njia za kutoa kipaumbele katika upatikanaji wa mtaji kwa watu wanaoshindana ili kuhakikisha uchumi unaweza kufikia ukuaji wa juu zaidi kwa gharama ya chini.

Muhimu zaidi, ni kuwa soko la hisa huwapa wawekezaji njia bora za kufanya uwekezaji wao kuwa wa kusonga kupitia hisa. Hali kwamba wawekezaji wana uhakika wa uwezekano wa kuuza mali wanayomiliki, wanavyotaka na wanapotaka, ni kichocheo kikuu kwa uwekezaji kwani huhakikisha urahisi wa kuhamisha mtaji katika ununuzi wa mali.

Utendakazi bora na kwa urahisi unaotokana na kuhamishwa kwa hisa unatarajiwa kufanya wawekezaji wengi kufurika katika soko la hisa. Hali sawa na iliyotokea baada ya kuanza kutumiwa kwa kompyuta katika uuzaji na ununuzi wa hisa inatarajiwa kushuhudiwa.

Mfumo wa kutumiwa kwa karatasi katika uuzaji na ununuzi wa hisa uliotumiwa hadi 2004 ulikuwa na changamoto nyingi ikiwa ni pamoja na kutolewa mara mbili kwa hisa, kupotea na kuharibiwa kwa vyeti vya hisa, kutooana kwa saini na pia kutumia muda mwingi. Hili lilikuwa likichangia kesi nyingi na mizozo kati ya wawekezaji. Kuanzishwa kwa CDSC kulibadilisha sana mambo katika sekta hii kwa kupunguza changamoto hizo na hatari zinazohusiana na vyeti vya karatasi kupitia kutoweza kusonga kwa hisa, na kuwezesha kukamilishwa kwa malipo na makubaliano kielektroniki katika soko la hisa. Kiasi cha kazi katika afisi nyuma ya kaunta kwa mawakala na benki za uwekezaji kilipungua sana kutokana na kuondolewa kwa haja ya kutumia mikono kuoanisha ununuzi na uuzaji wa stakabadhi za kubadilisha umiliki wa hisa na vyeti vya hisa.

Kutumiwa kwa kompyuta kulipunguza muda wa kukamilisha kwa ubadilishanaji kutoka siku 14- 21 awali hadi tatu pekee. Shughuli katika soko la mtaji Kenya sasa hukamilisha katika mzunguko T+3, matokeo ya moja kwa moja ya kutumiwa kwa kompyuta katika uuzaji na ununuzi na ubadilishanaji wa umiliki. Hasa, kuanza kutumiwa kwa CDS kulipunguza mzunguko wa kubadilisha umiliki kutoka zaidi ya T+7 hadi T+3 na hili limesaidia sana kuongeza shughuli katika soko kama inavyodhihirishwa na idadi ya shughuli za kibiashara zinazofanywa kila siku ambazo zinaongezeka kila uchao.

Ili kufanikisha kuhamishwa kwa hisa kutoka kwa vyeti hadi kwa orodha ya kielektroniki kwa awamu, kampuni zote zilizoorodheshwa kwenye NSE zimewekwa kwenye makundi matatu. Shughuli ya kuhamisha hisa ilianza 2012 kwa mashauriano kati ya wadau, warsha na mafunzo na hili litakamilika Novemba 2013.

Bi Mambo alifafanua kuwa matokeo ya kuhamishwa kwa hisa yatakuwa kwamba kuanzia tarehe ya kutekelezwa kwa shughuli hii, vyeti vya hisa havitatambuliwa tena kama ushahidi tosha wa umiliki wa hisa. Hata hivyo, wenyehisa hawana haja ya kuingiwa na woga kwamba watapoteza umiliki wao wa hisa kwani ushahidi wa umiliki wao utakuwa kwenye Central Depository System (CDS) ambayo huendeshwa na CDSC. Baada ya kutekelezwa kwa uhamishaji huu, hatari ambazo huwepo kutokana na kutumiwa kwa vyeti vya karatasi kwenye hisa zitaondolewa na sajili kamili ya wanachama katika kampuni iliyoorodheshwa itapatikana na kusimamiwa katika CDSC.

CDSC, alisema Bi. Mambo, "inachukua fursa hii kuwashukuru washirika wetu katika safari hii ya kuhamishwa kwa hisa hadi mfumo wa kielektroniki katika soko, Soko la Hisa la Nairobi na Mamlaka ya Masoko ya Mtaji, na pia ina shukrani nyingi kutokana na uungaji mkono iliopokea kutoka kwa wadau ikiwa ni pamoja na kampuni zilizoorodheshwa na wasajili wao wa hisa, pamoja na maajenti wetu wakuu wa uhifadhi wa hisa."

"Kuanzishwa kwa CDSC kulibadilisha sana mambo katika sekta hii kwa kupunguza changamoto na hatari zinazohusiana na vyeti vya karatasi kutokana na kutoweza kusonga kwa hisa, na kuwezesha kukamilishwa kwa malipo na makubaliano kielektroniki katika soko la hisa.